DARASA LA TANO

KISWAHILI

Jaza kifungu kifuatacho kwa kutumia jibu sahihi.

Watoto wengi ___1___ mitaani bila kufanya ___2___ cha maana. Wazazi wengi huogopa ___3___ . Watoto wanapozaliwa wengine ___4___ mapipani. Wasamaria wema hujitokeza ___5___ kuwasaidia kwa kuwapa makao, mavazi na vyakula. Watoto wengine hutorokea mijini kwa sababu ___6___ ya wazazi wao imevunjika. Wao huamua waende mjini wajitafutie kazi. Wanapofika huko wakati ___7___ mambo huharibika. Askari ___8___ wengine wakisingizia eti ni wezi. Wengi ___9___ huwa ni wavulana. Wasichana nao huwa na changamoto ___10___ . Baadhi yao ___11___ na baadaye kuambukizwa magonjwa ___12___ kama vile UKIMWI. Hali hii huwalazimu kuwa ___13___ kabla ya wakati wao kufika. Walioambukizwa huwa na afya ___14___ na baada ya kuugua kwa muda ___15___ dunia. Wazazi wanahimizwa kuwatunza wana wao.

1.	A. hawarandi	B. wanarandaranda	C. wanatembea	D. wanarukaruka
2.	A. lolote	B. yeyote	C. yoyote	D. chochote
3.	A. kuambiwa	B. majukumu	C. maneno	D. mambo
4.	A. hutupwa	B. hawatupwi	C. hupelekwa	D. hupewa
5.	A. ila	B. bora	C. ili	D. isipokuwa
6.	A. ndoa	B. doa	C. kuishi	D. usalama
7.	A. kwingine	B. pengine	C. mwingine	D. wengine
8.	A. hupenda	B. huchukia	C. huona	D. huua
9.	A. wao	B. yao	C. zao	D. chao
10.	A. jingi	B. nyingi	C. kingi	D. mingi
11.	A. huchapwa	B. huporwa	C. hunajisiwa	D. huambiwa
12.	A. mazuri	B. mabaya	C. sana	D. hatari
13.	A. wazazi	B. watoto	C. vijana	D. wazee
14.	A. nzuri	B. mzuri	C. baya	D. mbaya
15.	A. hutembea	B. huchukia	C. huaga	D. husalimu

Kutoka swali la 16 - 30 jibu kulingana na maagizo.

16. Kamilisha tashbihi:-
Mwaminifu kama _____
A. usiku B. malaika
C. mchana D. njiwa

17. Kanusha:-
Mimi nilisoma hisabati.
A. Wewe hukusoma hisabati.
B. Mimi sikusoma hisabati.
C. Mimi niliandika hisabati.
D. Mimi nilisoma kiingereza.

18. Mkuu wa wilaya huitwa:-
A. Disii B. Pisii
C. Chifu D. Dioo

19. Mtu anayefua vyuma huitwa:-
A. Seremala B. Mwashi
C. Sonara D. Mhunzi

20. Andika katika hali ya kutendewa.
Alijenga nyumba.
A. Alijengwa nyumba.
B. Alijengelewa nyumba.
C. Alijenga nyumba.
D. Alijengewa nyumba.

21. Maneno kama fua, vua, faa, vaa ni:-
A. vitate B. visawe
C. vitawe D. vivumishi

22. Malipo zaidi ya mkopo ni:-
A. fidia B. arshi
C. riba D. tuzo

23. Kamilisha:-
_____ ya ndizi.
A. Mkungu B. Chane
C. Shada D. Kicha

24. Andika kwa wingi.
Nyani ameruka mtini.
A. Nyani wameruka mitini.
B. Manyani wameruka mitini.
C. Manyani zimeruka mitini.
D. Nyani zimeruka mitini.

25. Andika kwa maneno $\frac{3}{9}$
A. tusui tatu
B. thuluthi tisa
C. subui tatu
D. tatu kwa tisa

26. Kamilisha methali:-
Afua ni mbili, _____
A. kuzaa na kulea
B. kusoma na kuajiriwa
C. kula na kulala
D. kufa na kupona

27. Mtoto wa nyuki huitwa:-
A. nyuki mdogo B. jana
C. malkia D. sega

28. Jina wanaloitana mke na ndugu wa kike wa mum ni:-
A. shangazi B. shemeji
C. wifi D. mkoi

29. Jina lingine la mkahawa ni:-
A. mbuni B. kawaha
C. kawa D. mchai

30. Jibu maamkizi:-
U hali gani?
A. vizuri B. mzuri
C. salama D. njema

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 31 - 40

Usafi ni kitu muhimu sana katika maisha ya kila mtu. Huchangia kufanikisha mambo mengi sana. Mambo haya humwezesha mtu kuishi bila wasiwasi wowote. Mwanafunzi akizingatia usafi na yuko darasan anaweza elewa kile mwalimu anafunza. Umewahi jiuliza uende shuleni bila kusugua meno, kisha umuonyes mwanafunzi mwenzako nini kinaweza tendeka?

Tuzingatie usafi wa mwili. Kila wakati mja anahimizwa aoge kwa maji na sabuni. Kufanya hivyo mv huwa safi. Unaposafisha mwili unajiepusha dhidi ya maradhi mengi ya ngozi. Pia unawezesha mwili kupata hewa safi. Tena unapotembea huna budi kuacha nyuma hewa safi. Mtu ambaye haogi hutoa harufu inayonuk kama kidonda. Sote tujuavyo tungependa kuishi bila harufu mbaya. Hata meno yanafaa kusafishwa kila siku Ikiwezekana mara tatu kwa siku.

Tusisahau usafi wa mazingira. Mahali unaenda hakikisha kuwa unadumisha usafi. Baada ya kula matunda tafuta mahali panapostahili kabla utupe uchafu. Kwa mfano mtu anaweza kula ndizi kisha atupe ga lake, kando na kuchafua mazingira mwingine anaweza kuja na kuanguka. Jameni kila mtu atupe taka mahal panapostahili.

Hata shuleni usafi ni wa maana. Kwa mfano darasani wanafunzi watupe takataka ya kila aina kisha baadaye wakose kutoa. Darasa hilo haliwezi kukalika kamwe. Uyando unaweza fanya wanafunzi wakose kuwasikiliza walimu. Hata wadudu wanaweza tembea madarasani. Jambo hili linafaa kutiliwa maanani kwa bila usafi vitu vinaweza kuharibika.

Bila kusahau vyakula tunavyovila vinafaa kuwa safi. Tukila vyakula vichafu tunaweza kuwa wagonj Matibabu kwa ajili ya kula vyakula vichafu huwa ghali. Vyakula kabla viliwe lazima viwe vimezingatia us Mahali ambapo vinapikiwa lazima kuwe safi. Kabla ule matunda unalazimishwa kuosha.

Sote tudumishe usafi ili maisha yawe bora. Kama tujuavyo usafi una manufaa mengi. Baada ya kuto msalani osha mikono kwa maji pamoja na sabuni. Tushirikiane ili tuendeleze usafi.

Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.0.Box 85726-00200, Nairobi. Tel:+254202319748 | +254733836593 | email: infosnkenya@gmail.com. Order answers online at: www.schoolsnetkenya.com

31. Kulingana na aya ya kwanza ni nini kinamwezesha mtu kufanikisha mambo mengi?
A. Usalama
B. Usafi
C. Uchafu
D. Nyumba nzuri

32. Neno mja kama lilivyotumika kwenye ufahamu linamaanisha:-
A. mdudu
B. mnyama
C. ndege
D. mtu

33. Nuka kama kidonda ni fani gani ya lugha?
A. tashbihi
B. methali
C. istiara
D. semi

34. Usafi wa shuleni unachangia vipi katika masomo?
A. Kutoelewa kwa mwanafunzi
B. Kusoma kwa taabu
C. Kuelewa kwa wanafunzi
D. Kuhisi uvundo darasani

35. Ni nini kinaweza oshwa kabla ya kuliwa?
A. Peremende
B. Vibanzi
C. Maembe
D. Ugali

36. Ni methali ipi inaweza kutumika kuonyesha ushirikiano?
A. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
B. Haba na haba hujaza kibaba
C. Jungu kuu halikosi ukoko
D. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu

37. Kinyume cha nuka ni:-
A. nukua
B. nukia
C. usinuke
D. hainuki

38. Ni sentensi gani sahihi kulingana na ufahamu?
A. Mwanafunzi safi hawezi fanya vyema katika mtihani
B. Usafi ni wa watu walio na pesa
C. Usafi huchangia kuboresha afya
D. Tunawe mikono kabla ya kwenda msalani

39. Ugonjwa upi unaweza tokana na kula vyakula vichafu?
A. Malaria
B. Homa
C. UKIMWI
D. Waba

40. Kichwa mwafaka cha taarifa hii ni:-
A. Udumishaji wa usafi
B. Udunishaji wa usafi
C. Kuendeleza uchafu
D. Hasara za usafi

Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali nambari 41 - 50

Katika kijiji kimoja, kuliishi mzee Karimu pamoja na mkewe mkongwe. Walikuwa wamekula chumvi mno. Walikuwa pamoja na wajukuu wao watatu. Mkewe hakuwa na kazi yoyote lakini mzee Karimu alifanya kazi ya uvuvi. Wazazi wa wajukuu hao waliaga dunia kutokana na ajali mbaya ya barabarani. Hawakuwa na budi ila kuwasaidia. Alikuwa akipata mapato madogo. Wakati mwingine wangelazimika kulala njaa.

Siku moja walitembelewa na mgeni asiyekuwa wa kawaida. Alidai ya kwamba alikuwa akihisi njaa k Walimpa mlo kisha akala kwa ulafi wa fisi. Alipomaliza alisema ya kwamba hakuwa ameshiba. Walishangaa kwani chakula kilikuwa kidogo. Walimbembeleza alale kwani methali waliyokuwa wakiiamini kuwa mgeni njoo mwenyeji apone haikutimia. Ilikuwa sasa mgeni njoo mwenyeji awe na huzuni. Baadaye aliomua kulala

Familia hiyo ilipata fursa ya kupika chakula chao hata nao wale. Baada ya kushiba walienda kulala. Tukio la ajabu lilitokea. Watu wawili walikuja kwa mzee Karimu na magari ya kifahari. Walikuwa wakimtafi yule mgeni aliyewatembelea. Walishangaa ni vipi waliweza kumlisha na jinsi hali yao ilivyokuwa. Mzee Karimu aliwaeleza kuwa walimpa chakula kisha wakambembeleza akalale. Walifurahi kama mfalme. Walimshukuru mzee Karimu kwa ukarimu wake na kumpa vyakula vingi.

Baadaye hawakumwacha hivyo bali walimpa kazi iliyomlipa shilingi elfu ishirini kwa mwezi. Furaha

ake haikuwa na kikomo. Wajukuu pia walichukuliwa na kupelekwa shule. Kama hangemsaidia yule mgeni aisha yake hayangebadilika. Kuwa na moyo wa ukarimu hukuzalia matunda. Methali ya mgeni njoo mwenye pone ikatimia.

Alipofanya kazi alionyesha bidii mno kuliko hata umri wake. Alikuwa mwaminifu na waliomwajiri akaamua kumpandisha cheo. Kutoka hapo familia hiyo iliinuka sana.

---

41. Ni nini maana ya kula chumvi?
A. kumeza chumvi
B. kuzeeka
C. umri mdogo
D. vijana

42. Watu wangapi wametajwa kwenye ufahamu?
A. tisa
B. nane
C. kumi na moja
D. kumi

43. Mzee Karimu alifanya kazi gani?
A. uvivu
B. uvuvi
C. udaktari
D. uhandisi

44. Mzee Karimu hakuwa na sifa gani?
A. mchoyo
B. karimu
C. mapenzi
D. mwenye bidii

45. Kamilisha tashbihi:-
Mwaminifu kama _____
A. malaika
B. paka
C. mchana
D. usiku

46. Mgeni alilala wakati gani?
A. mchana
B. usiku
C. asubuhi
D. hatujaambiwa

47. Mwanzoni familia hii ilikuwa katika hali gani?
A. utajiri
B. ubwanyenye
C. umwinyi
D. umaskini

48. Ni kweli kusema:-
A. familia hiyo ilibaki maskini hadi mwisho
B. mgeni alileta hasara hadi mwisho
C. familia hiyo iliishia kuwa ya matajiri
D. mzee Karimu na mkewe hawakuwa maskini

49. Kwa nini mzee Karimu alipandishwa cheo?
A. Alikuwa mwaminifu
B. Alikuwa na bidii
C. Ilikuwa desturi
D. Alihongana ndiposa akapandishwa

50. Kichwa mwafaka cha taarifa hii ni:-
A. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
B. Fuata nyuki ule asali.
C. Chelewa chelewa utampata mwana si wako.
D. Mgeni njoo mwenyeji apone.

Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.0.Box 85726-00200, Nairobi. Tel:+254202319748 | +254733836593 | email: infosnkenya@gmail.com. Order answers online at: www.schoolsnetkenya.com